# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la kwanza na la pili

Mfululizo wa A
Masomo ya saba hadi kumi na mbili

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya "Wakati na Biblia/Bibletime", "Maisha Mapya/New Life" na "Wakusanyaji/Gleaners" kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wamechukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wakufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa na vikundi mbalimbali kutoka makanisa na shule mbalimbali ambavyo vimezingatia mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na yanamruhusu mwanafunzi kuyatumia kwa muda mrefu hadi atakapotimiza umri wa miaka ishirini. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (chini ya miaka mitano), miaka mitano hadi saba, miaka nane hadi kumi, miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu na miaka kumi na minne hadi kumi na sita. Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 6). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongonzo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwa mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES


**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo wa kufundisha umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo wa kufundisha katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya daraja la kwanza na la pili kwa watoto wenye umri wa wastani wa miaka 5-10.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kwa kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Hatupendi kutoa shinikizo na kutokuwapa waalimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri –** Waalimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza –** Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Waalimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi –** Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha –** Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba waalimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze –** Kuna Mstari muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha –** Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu uwepo ili watoto wasichukulie masomo kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka –** Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha –** Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Viunga (links) maalum vya tovuti ya Free Bible Images kwa ajili ya Masomo yote ya daraja zote na mfululizo wote wa Wakati na Biblia yanapatikana kwa barua pepe kutoka kwenye ofisi ya BES. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kufundisha Mstari Muhimu

1) Mstari unafaa kuandikwa kwenye karatasi au ubaoni na baadhi ya maneno kuondolewa huku watoto wakirudia ule mstari hadi pale maneno yote yatakapoondolewa na watoto kuurudia mstari bila kuangalia maneno.
2) Ili kuwaanzishia watoto Mstari muhimu, mwalimu anaweza kutumia:
   a) Njia ya Hangman yenye vikundi viwili (2 teams) – Unaweza kuwapa watoto baadhi ya nafasi za herufi za ule Mstari muhimu bila herufi zenyewe – Watoto watachagua herufi wanazozitaka mpaka mtu atakapoweza kuuona Mstari muhimu.
   b) Njia ya Sword Drill – watoto wanakuwa na Biblia na wote wanashindana kutafuta mstari huo wa Biblia na atakayeupata wa kwanza ataruhusiwa kuusoma kwa sauti.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
  1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
  2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi10
  3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
  4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0 (Chekechea/Chini ya miaka mitano) Daraja la Kwanza (Miaka mitano hadi saba) Daraja la Pili (Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

# A7 Habari ya kwanza

**Petro akihubiri – Habari hii inahusu Petro akisaidiwa na Roho Mtakatifu kuhubiri kuhusu Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Ilikuwa muhimu kwa wanafunzi kuwa na Roho Mtakatifu.<br>• Roho Mtakatifu anaishi ndani ya kila mtu aliyemwamini Bwana Yesu kama Mwokozi.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 2:36***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 2:1-14, 36-39*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Tumia maswali kumtambulisha Roho Mtakatifu. Je, unaweza kuona upepo? La! Je, unajuaje kuna upepo? Unaweza kuona vitu ambavyo upepo unasababisha. Kama unaweza kuona nje, tafuta uthibitisho wa vitu vinavyosababishwa na upepo.<br>• Wakumbushe watoto kuhusu habari ya siku ya kukumbuka kifo na kufufuka kwa Yesu. Kabla hajaondoka kwenda mbinguni, aliwaahidi wanafunzi wake msaidizi maalum sana ambaye asingeonekana kwa macho.<br>• Msaidizi huyu aliitwa Roho Mtakatifu. Angekuja na kuishi kwa kila mmoja wao. Kama upepo, hawangeweza kumuona lakini wangepata utofauti ambao angeleta kwenye maisha yao. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja muda mfupi baada ya Yesu kwenda mbinguni, wanafunzi walikuwa wamekusanyika kwenye nyumba moja kule Yerusalemu. ***(Matendo 2:1-4)*** Kwa ghafla, nyumba ile ikajawa na sauti kuu ya upepo wa kasi. Kisha kitu kama ndimi za moto vikakaa juu ya kichwa cha kila mmoja. Roho Mtakatifu alikuwa amekuja! *Je, unafikiri mitume walijihisi vipi kwa sababu sasa walikuwa wamepata kipawa maalum? (walifurahi, walistaajabu, walifurahi kuwa ahadi ya Mungu ilikuwa imetimia)*<br>• Kisha, wakagundua kuwa walikuwa wananena kwa lugha tofauti! *Elezea kuwa, kwa kawaida tunaweza kuzungumza lugha tuliyojifunza kutoka kwa wazazi wetu tulipokuwa wadogo au tuliyofundishwa. Wanafunzi wa Yesu hawakuwa wamefundishwa lugha hizo.* Ishara hizi zote zinaonesha kuwa Roho Mtakatifu alikuwa amekuja. *Je, ungefikiri nini kama ulikuwa unatembea karibu na chumba walimokuwemo?*<br>• Watu waliokuwa karibu na mahali pale walishangaa! ***(Matendo 2:5-13)***<br>• Petro alijua kuwa, hii ilikuwa fursa yake ya kuelezea kilichokuwa kinafanyika na kuwaambia kuhusu Bwana Yesu. ***(Matendo 2:36-39)*** *Jadili kwanini ilikuwa vigumu kuuhubiria ule umati mkubwa. (Lilikuwa jambo la kuogopesha, kutojua maneno sahihi yakutumia, kujali watu wangewaza au kufanya nini ...)* Lakini Petro aliweza kuhubiri kwa sababu alisaidiwa na Roho Mtakatifu.<br>• *Wale waliokuwa wanamsikiliza Petro iliwabidi kuokolewa kutoka kwa dhambi zao. Nasi pia tunahitaji kuokolewa.*<br>• *Elezea kuwa, kila anayemwamini Bwana Yesu kama Mwokozi anapokea Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu atatusaidia kuwaambia wengine kumhusu Yesu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – The day of Pentecost. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Matendo 2:36***. Hii ni sehemu ya kile ambacho Petro alisema alipokuwa anahubiri. Aliwaambia kuwa, wao ni watu waliokuwa wamemuua Yesu lakini Mungu alimfufua. Hii ilidhihirisha kuwa, Yesu hakuwa mtu tu, alikuwa Bwana na Kristo. |
| **KUMBUKA** | • Mitume walikuwa wapi Roho Mtakatifu alipowashukia?<br>• Roho mtakatifu alisikika kama nini?<br>• Mitume waliona nini?<br>• Je, waliweza kufanya nini mara tu walipojazwa na Roho Mtakatifu?<br>• Ni mtume yupi aliyesimama na kuelezea kilichokuwa kimetokea?<br>• Petro aliongea kumhusu nani?<br>• Je, Petro aliwaambia wafanye nini kuhusu dhambi zao?<br>• Je, wangepokea zawadi gani kama wangefanya hivyo?<br>• Ni watu wa aina gani wana Roho Mtakatifu ndani yao siku za leo? |

## A7 Habari ya pili
**Petro amponya kiwete – Habari hii inahusu nguvu za Mungu za uponyaji.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Nguvu za Yesu zilifanya kazi kupitia Petro na Yohana kumponya yule mtu kiwete.<br>• Petro na Yohana walitaka kumsaidia yule mtu kiwete na inatupasa kujaribu kuwasaidia wengine pia.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Daraja la Kwanza-Matendo 3:6, Daraja la pili-Matendo 3:16***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 3:1-12*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Kwa umakini, elezea mtu yule kiwete ambaye asingeweza kutembea lakini alikete malangoni pa hekalu na kuwaomba watu hela ili kununua chakula na ili kujikimu maishani.<br>• Kama unaweza kupata, waoneshe watoto magongo. Lakini elezea kuwa, mtu huyu ilibidi abebwe na rafiki zake.<br>• Tumia mchoro wa uso wa huzuni kuonesha uso wa yule mtu. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja Petro na Yohana walipokuwa wakienda hekeluni, yule kiwete akawaaomba hela. ***(Matendo 3:1-5).*** *Elezea kuwa, walitumia muda na kuwa naye.*<br>• Tumia maneno ya Petro. “Fedha na dhahabu sina. Lakini nitakupa nilichonacho. Kwa Jina la Yesu, simama uende!” ***(Matendo 3: 6-7)*** *Elezea kuwa, fedha na dhahabu zingemsaidia yule mtu kwa muda mfupi- haingeweza kufanya miguu yake kutembea.* Petro aliweza kumpa kitu ambacho kingebadilisha maisha yake kabisa.<br>• Petro akashika mkono wake na akamsaidia kusimama. Kwa ghafla, miguu ya yule mtu ikipata nguvu. Akaweza kutembea na kuruka–ruka kwa mara ya kwanza maishani mwake! Akamsifu Mungu na akaendelea kuwe kule hekaluni pamoja na Petro na Yohana. ***(Matendo 3:8)*** *Onesha mchoro wa uso wenye furaha, kinyume na ule uso wa hapo awali. Je, ungewaza nini kama ungekuwa umezoea kumwona yule kiwete akiomba hela na sasa alikuwa anatembea?*<br>• Kila mtu alishangazwa na yaliyokuwa yametokea. ***(Matendo 3: 9-12)***<br>• *Fikiria jinsi gani tunaweza kufuata mfano wa Petro. Ongea kuhusu kuwasaidia wengine kwa namna halisi au njia inayowezekana. Pia unaweza kuwaambia wototo kuwa, jambo muhimu zaidi ambalo tunaweza kuwashirikisha wengine ni Habari Njema ya Bwana Yesu.*<br>• *Kama yule mtu, sisi pia tuna shida maishani mwetu. Nguvu za Yesu zinaweza kutuondolea dhambi kama vile yule mtu aliwekwa huru kutoka kwa ile hali ya kutoweza kutembea.*<br>• *Fikiri kuhusu mambo ambayo yatatusababisha kumwabudu Mungu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – A lame beggar is healed. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – **Daraja la Kwanza - *Matendo 3:6,* Daraja la Pili - *Matendo 3:16.*** *Kama inafaa, watoto wanaweza kusema ule Mstari muhimu wakitembea au wakirukaruka.* |
| **KUMBUKA** | • Ilikuwa ni wakati gani?<br>• Petro na Yohana walikuwa wanaenda wapi?<br>• Yule mtu alikuwa hawezi kutembea kwa muda gani?<br>• Je, aliketi wapi kila siku?<br>• Je, aliwaomba Petro na Yohana nini?<br>• Je, Petro alitumia Jina la nani kumponya yule mtu?<br>• Je, Petro alifanya nini kingine baada ya kuongea na yule mtu?<br>• Taja mambo matatu ambayo mtu yule aliweza kuyafanya?<br>• Je, yule mtu alienda wapi baada ya kupona?<br>• Je, nguvu za Yesu zinaweza kufanya nini maishani mwetu? |

## A7 Habari ya tatu

**Petro akiwa gerezani – Habari hii inahusu jinsi Mungu anavyowasaidia wale wanaomtumikia.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Wakristo wa kwanza walikutana na vipingamizi kutoka kwa viongozi wa dini waliokuwa wamemsulubisha Bwana Yesu.<br>• Wale wanaompenda Yesu kwa mioyo yao yote watapenda kumtii hata wakati wa matatizo.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 13:6***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 4:1-22*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Kwa sababu habari hii ni mwendelezo wa habari ya hapo awali, ni vyema kuyarudia baadhi ya mambo ya habari hiyo.<br>• Tumia michoro ya uso wa huzuni na pia ule wa uso wa furaha.<br>• Je, yule mtu alikuwa amefanyiwa nini ili kuweza kutembea? Hakikisha kuwa watoto wanaelewa kwamba ilikuwa kwa kupitia nguvu za Yesu yule mtu alipona. |
| **FUNDISHA** | • Baada ya haya, Petro na Yohana walihubiri kuhusu Yesu aliyekuwa amefufuka na watu wengi wakaamini. ***(Matendo 4:1-2, 4)*** Lakini wale wakuu wa masinagogi wakakasirika kwa sababu Petro aliwaambia watu kuwa Yesu alikuwa amefufufka. Punde tu, Petro na Yohana wakakamatwa na kutiwa gerezani. ***(Matendo 4:3)*** *Elezea jinsi gani Petro na Yohana walilichukulia jambo hili.*<br>• Asubuhi, wakapelekwa mahakamani na kuulizwa maswali. ***(Matendo 4:5-7)*** *Elezea kuwa, mahakama ni kundi la watu wanaoamua ikiwa mtu amekosa.*<br>• Kwa mara nyingine, Petro alisaidiwa na Roho Mtakatifu kuelezea jinsi gani yule mtu aliponywa. ***(Matendo 4: 8-12)*** Mahakama ilishindwa iwafanyie nini Petro na Yohana! Walijua kwamba muujiza mkubwa ulikuwa umetokea lakini baada ya kuujadili, wakafanya uamuzi na wakawaambia Petro na Yohana wasiongee tena kuhusu Yesu. ***(Matendo 4:13-19)*** *Je, Petro na Yohana wangehisi nini kuhusu jambo hili? Je, wangetii?*<br>• Petro na Yohana walijua kwamba haitawezekana wao kuacha kuongea Habari za Yesu! ***(Matendo 4:20)*** *Walimpenda Yesu sana na waliamua kumtii. Walijua kuwa, wakimtumainia Yesu atakuwa pamoja nao kwa kila hali. Roho Mtakatifu atawasaidia.*<br>• *Yesu anataka tumpende na kumtii hata kama ni kwa hali ngumu kiasi gani.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Peter and John are arrested. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Waebrania 13:6***. Unaweza kucheza “Hangman”kwa kutumia maneno matano ya kwanza kabla ya kuongeza vile visehemu vingine viwili. Watoto wanaweza kugawanywa katika makundi matatu na kila kikundi kukariri kisehemu na wote kurudia kusema ni mstari upi… yaani waebrania 13:6. *Je, unafikiri maneno haya yangewasaidia Petro na Yohana? Elezea kuwa, watoto wakiyajua yanaweza kuwa msaada kwao!* |
| **KUMBUKA** | Kuwa na maswali ya KWELI au SIYO KWELI na sentensi zilizoandikwa kwenye vikaratasi na kuwekwa kwenye mfuko. Kila sentensi iwe na maksi, (5 hadi 100). Uwe na vikundi kiwili.<br>• Wale askari walikasiriswa sana na Petro na Yohana.<br>• Walikaa usiku mmoja gerezani.<br>• Walipoachiliwa, waliulizwa maswali na mahakama.<br>• Petro aliiambia mahakama kuwa, Nguvu za Yesu zilikuwa zimemponya yule mtu.<br>• Roho Mtakatifu alimsaidia Petro na Yohana kuongea na mahakama.<br>• Petro na Yohana walitoroka kutoka mahakamani.<br>• Mahakama iliamua kuwa, Petro na Yohana wasinene tena kuhusu Yesu.<br>• Petro na Yohana walisema kuwa, watatii ile mahakama. |

## A7 Habari ya nne

**Petro afunguliwa – Habari hii inahusu Mungu kujibu maombi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu anatoa nguvu zake na kuwasaidia wakristo ili wafanye kazi yake.<br>• Maombi ni muhimu kwa kila hali tunayoipitia.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 4:31 au Mathayo 6:33***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 4:23-31*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu habari ambayo watoto wangependa kushiriki na marafiki au jamaa – inawezekana ni habari ya kusisimua kuhusu walichokifanya walipoenda kwenye" sherehe au kambi ya watoto" au kushinda kwenye mashindano. Au kuhusu jambo fulani walilokuwa na hofu nalo lakini wakapata msaada walipowashirikisha marafiki. |
| **FUNDISHA** | • Petro na Yohana walikuwa na habari ya kuwashirikisha marafiki. ***(Matendo 4:23)*** Elezea kuwa, habari hii njema ilikuwa inawahusu wao kutoka gerezani lakini habari mbaya ilikuwa ni kukatazwa kunena Habari za Yesu!<br>• Marafiki wa Petro na Yohana wakafanya uamuzi wa busara kuomba. ***(Matendo 4:24-30)*** Walijua kuwa, Mungua alikuwa anatawala. Alikuwa mkuu zaidi ya wale watu waliokuwa wamejaribu kuwakataza kuhubiri. Walipoomba, walikumbuka mambo ya ajabu ambayo Mungu alikuwa ameyafanya yaliyodhihirisha nguvu zake. Wakamwomba Mungu awape ujasiri na kufanya miujiza zaidi kwa nguvu za Yesu. ***(Matendo 4: 29,30)***<br>• Punde tu walipoomba, Mungu alijibu Maombi yao! ***(Matendo 4: 31)*** *Elezea kuwa, jengo lilitikisika kwa sababu Mungu alikuwa anawaonesha nguvu za Roho Mtakatifu kwa mara nyingine. Roho Mtakatifu alikuwa nao na angewasaidia wanaponena kuhusu Bwana Yesu.*<br>• *Elezea kuwa tunaweza kumwomba Mungu tunapokuwa na mambo magumu ya kufanya.*<br>• *Mungu anasikia na kujibu maombi yetu na atatusaidia kumpa Bwana Yesu kipaumbele, kama wale watu kwenye habari ya leo.*<br>• *Kwa watoto wa daraja la pili, unaweza kuwaambia kuhusu Wakristo wanoishi kwenye nchi ambazo wanakatazwa kuongea kuhusu Habari Njema ya Bwana Yesu. Tunaweza kuwaombea wapewe ujasiri wakumpa Bwana Yesu kipaumbele.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Peter and John are arrested. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Matendo 4:31 au Mathayo 6: 33. Kwenye Mathayo 6:33***, Neno "kutafuta" linamaanisha kuweka. Ufalme wa Mungu unamaanisha kila kitu ambacho ni muhimu kwa Mungu na kinachomhusu Bwana Yesu. |
| **KUMBUKA** | Kuwa na maswali yanayogusia habari zote za A7<br>• Kwa nini wanafunzi wa Yesu walimhitaji Roho Mtakatifu?<br>• Je, wanafunzi waliona nini Roho Mtakatifu alipowashukia?<br>• Malizia Mstari muhimu: "Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa _______ na __________." ***(Matendo 2:36)*** [Habari ya Kwanza ]<br>• Kwa nini yule mtu alikuwa anaomba hela hekaluni?<br>• Alikuwa hajatembea kwa muda gani?<br>• Kamilisha kwa kuweka maneno yaliyokosekana kwenye Mstari muhimu: "Kwa Jina la Yesu Kristo , _________ ________."<br>• Je, muujiza huu uliwadhihirishia watu nini kuhusu Bwana Yesu?<br>• Kwa nini Petro na Yohana walitiwa gerezani?<br>• Mahakama iliwaamuru wasifanye nini?<br>• Nini kilitokea Mungu alipojibu maombi ya marafiki wa Petro na Yohana? |

<u>**A8 Habari ya kwanza**</u>

**Petro amsaidia Dorkasi – Habari hii inahusu kumfufua Dorkasi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Nguvu za Bwana Yesu zilitenda kazi ndani ya Petro alipomponya Dorkasi.<br>• Inatupasa kumuitikia Bwana Yesu kwa kumuamini.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 9:42***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 9:32-43*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Ongea kuhusu njia ambazo tunaweza kuwasaidia watu wenye shida kwa kuwapa tulivyonavyo. Kama inawezekana, tumia picha au igizo kuonesha jinsi ya kufanya hivi.<br>• Mtambulishe Dorkasi kama mwanamke mkarimu sana aliyempenda Bwana Yesu. Kwa sababu ya hili, alitumia muda wake kuwasaidia wengine na alikuwa ana ujuzi wa kushona nguo na nguo hizo aliwapa maskini. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja, Dorkasi akaumwa na kufa. ***(Matendo 9:37)*** *Je, rafiki zake walihisi vipi?*<br>• Wakristo wawili wakaenda kumtafuta Petro aliyekuwa mji jirani uitwao Yafa. ***(Matendo 9:38, 39)***<br>• Mara moja, Petro akaenda nyumbani mwa Dorkasi. ***(Matendo: 9:40, 41)*** *Elezea kwa undani Petro alivyoomba, kisha akaongea naye, baadaye akamshika mkono na kumsaidia kusimama. Dorkasi akafufuka! Tofautisha hali hii ya furaha na mazingiza ya huzuni ambayo Petro alikutana nayo alipofika nyumbani mwa Dorkasi. Sisitiza kuwa huu ulikuwa muujiza ambao Petro angeweza kuufanya kwa nguvu za Bwana Yesu tu zilizokuwa zinafanya kazi ndani yake.*<br>• Watu wengi wakamwamini Bwana Yesu. ***(Matendo 9:42)***<br>• *Tunahitaji kumwamini Bwana Yesu kama wale waliomwona Dorkasi akifufuka.*<br>• *Elezea kwa ufupi hili linamaanisha nini – lazima tutambue kuwa, Yeye Ni Mwana WA Mungu, Yu hai na ana uwezo wakutuondolea dhambi. Kumwamini Yesu kunamaanisha kuwa, tunamtumainia kwa vyote.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI –Tabitha Dorcas is raised to life. |
| **JIFUNZE** | Fundisha Mstari muhimu – ***Matendo 9:42***<br>*Mstari huu muhimu utakuwa rahisi hata kwa wale watoto wa umri mdogo – kwa mara nyingine, hakikisha kuwa watoto wameuelewa. Hakikisha wameelewa “wengi” ni akina nani. Ni nini kilichowafanya wamwamini Bwana? Kwa nini ni muhimu kwetu sisi kumwamini Bwana? Mtu atamwaminije Bwana?* |
| **KUMBUKA** | • Dorkasi aliishi wapi?<br>• Je, aliwasaidia watu kwa njia gani?<br>• Kwa nini aliwasaidia watu?<br>• Je, watu walihisi nini Dorkasi alipokufa?<br>• Je, ni nani aliyeenda kumtafuta Petro?<br>• Petro alifanya nini alipopiga magoti mahali ambapo Dorkasi alikuwa amelala?<br>• Je, Petro alimwambiaje Dorkasi?<br>• Petro alifanya nini baada ya kuongea na Dorkasi?<br>• Je, watu wengi walifanya nini baada ya Dorkasi kufufuka?<br>• Mstari muhimu unapatikana wapi? |

## A8 Habari ya pili

**Petro apata maono – Habari hii inahusu upendo wa Mungu kwa kila mmoja.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Petro alitii maagizo ya Mungu.<br>• Mungu anampenda kila mtu na anataka kila mtu ajue Habari Njema ya Bwana Yesu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Yohana 3:16***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 10:9-23*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Ongea kuhusu jinsi ambavyo watu wa nchi tofauti/ maeneo tofauti duniani wanavyotofautiana - Tumia picha kama inawezekana.<br>• Ongea kuhusu utofauti wa rangi ya ngozi, nywele, lugha na kadhalika.<br>• Mungu aliumba kila mmoja. Anataka kila amjue na pia ajufunze kuhusu Mwana wake, Bwana Yesu. |
| **FUNDISHA** | • Petro alipokuwa akiomba kule Yafa (husisha habari hii na ile ya kwanza kwenye A8) Mungu alimfundisha Petro ampende kila mtu ***(Matendo 10: 9-16)*** *Hamna haja ya kuzungumzia maono hayo kwa undani. Kwa watoto wa Daraja la pili, unaweza kuelezea kuwa, ukweli huu ulikuwa mgumu kwa Petro kuuelewa kwa sababu alikuwa Myahudi na hadi wakati ule, aliamini kuwa, ni wayahudi tu waliokuwa wa muhimu mbele za Mungu. Ilibidi Petro ajifunze kuwa, kila mtu ni muhimu mbele za Mungu.*<br>• Wageni watatau wakawasili na wakamwomba Petro aambatane nao hadi nyumbani kwa Kornelio. ***(Matendo 10:17-22)*** *Elezea kuwa, Kornelio alikuwa akida au afisa muhimu wa jeshi la Kirumi aliyekuwa makini kujua zaidi habari za Mungu.* Korinelio na Petro walikuwa ni watu wa aina tofauti na kwa kawaida, haikuwa rahisi kwa Petro kwenda kumtembelea mtu kama Kornelio. *Elezea jinsi gani Petro alijua kuwa, ilimpasa kwenda (1) kupitia yale ambayo Mungu alikuwa amemfundisha (2) kupitia uongozi wa Roho Mtakatifu.*<br>• Petro akasafiri hadi nyumbani kwa Kornelio huko Kaisaria. (Takribani umbali wa maili 40) ***(Matendo 10:23)*** *Jaribu kuelezea umbali huu na umbali ambao watoto wanaujua au wanaweza kuutambua. Inawezekana safari hii ilichukua siku nzima. Sisitiza utii wa Petro mbele za Mungu alipoifanya safari hii.*<br>• *Sisitiza kuwa, Mungu anataka kila mtu ajue kuwa, anampenda. Alimtoa Mwanawe afe msalabani ili kila mtu asamehewe.*<br>• *Kama umemwamini Bwana Yesu, basi unaweza kuwasaidia wengine kumjua.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Peter tells Cornelius about Jesus. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Yohana 3:16*** |
| **KUMBUKA** | • Petro alikuwa anakaa na nani?<br>• Petro alikuwa anafanya nini saa za mchana?<br>• Je, Mungu alitaka Petro ajue nini alipoongea naye?<br>• Ni watu wangapi waliokuja kumwita Petro?<br>• Je, Petro alitaka kumtembelea nani?<br>• Kornelio alikuwa anafanya kazi wapi?<br>• Kwa nini Petro alienda nyumbani mwa Kornelio?<br>• Mungu alionesha vipi kuwa alimpenda kila mtu duniani?<br><br>**Igiza:** Sehemu ya habari ambapo wageni wanafika inaweza kuigizwa na kuendelezwa kwenye habari ya tatu. Watu wazima au Viongozi wa darasa wanaweza kuigiza sehemu ya Wageni na Petro. |

**<u>A8 Habari ya tatu</u>**
**Petro na Kornelio – Habari hii inahusu Mungu kuokoa afisa wa jeshi la Kirumi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Kornelio alikuwa mtu wa kwanza asiyekuwa Myahudi (mtu wa mataifa) kumwamini Yesu na jinsi jambo hili lilitokea.<br>• Mungu yupo tayari kusamehe dhambi za kila anayemwamini.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 10:43***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 10:23-48*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Kwa sababu huu ni mwendelezo wa habari ya wiki iliyopita, ni muhimu kutumia baadhi ya maswali kutoka kwenye Habari ya pili ili kurudia matukio.<br>• Baada ya kufanya hivi, unaweza kuwaambia watoto kuhusu tukio kwenye jamii yenu ambapo watu hukusanyika ili kupata habari. |
| **FUNDISHA** | • Petro akafika nyumbani mwa Kornelio. ***(Matendo 10:24-33)*** *Wasaidie watoto kufikiri kuhusu mkusanyiko wa watu – nyumba iliyojaa jamaa na marafiki wa Kornelio na kila mtu akiwa makini kumtazama Petro.* Kornelio alimchukulia Petro kama mgeni maalum sana kwa hiyo akamsujudia. Petro akamwambia ainuke kwani haikuwa sahihi kumsujudia mtu wa kawaida. Kisha Kornelio akaelezea kuwa ni Mungu aliyekuwa amemuelekeza kumwita Petro. Unaweza kuelezea kuwa Mungu alikuwa amewaanda wote wawili kwa ajili ya mkutano huu!<br>• Ujumbe wa Petro. ***(Matendo 10:34-43)*** *Elezea jinsi Petro alivyowaambia kuwa, Mungu anataka watu kutoka kwenye mataifa yote wamuamini.*<br>• *Zungumza kuhusu maneno ya Petro kumhusu Bwana Yesu – alivyosababisha mambo mazuri, kuwaponya watu, alivyouawa na Mungu akamfufua. Siku moja, Bwana Yesu atahukumu watu, lakini cha muhimu ni kuwa, anatoa msamaha wa dhambi kwa kila amwaminiye sasa.*<br>• Mwitikio wa wale wasikilizaji. ***(Matendo 10:44-48)*** Roho Mtakatifu aliwasaidia watu hawa kuelewa ujumbe Petro. Walimwamini Bwana Yesu na dhambi zao zikasamehewa.<br>• *Elezea kuwa, tukisikia Habari Njema za Bwana Yesu, inatupasa kumwitikia kama watu hawa. Kwa kumwamini, sisi pia tutasamehewa dhambi zetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Peter tells Cornelius about Jesus. |
| **JIFUNZE** | Kama infaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Matendo10:43***. *Elezea maana ya “Yeyote” na “kusamehewa”.* |
| **KUMBUKA** | Badala ya maswali zaidi, itakuwa wazo zuri ikiwa watachora nyuso zao pembeni mwa Mstari muhimu ukiwa umeandikwa kwenye bango na kwa maandishi makubwa. Kila mtoto achore uso wake. Hii itasaidia kusisitiza ukweli wa upendo wa Mungu ambao Petro alikuwa amejifunza. Pia itawasaidia kuelewa kuwa “kila mmoja” inamaanisha wao pia. Njia nyingine, watoto wanaweza kukata picha za nyuso tofauti kutoka kwenye magazeti yaliyotumika kama yanaweza kupatikana.<br><br>**Igiza:** Kama ilivyopendekezwa kwenye habari ya pili, sehemu hii pia inaweza kuigizwa. |

## A8 Habari ya nne

**Petro akiwa gerezani tena – Habari hii inahusu Mungu kujibu maombi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Rafiki za Petro walimuombea.<br>• Mungu anaweza akaamua kufanya mambo ya ajabu kama jibu la maombi yetu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Yakobo 5:16***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 12:1-19*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Ongea kuhusu kutumia simu na kuongea na marafiki zetu au kumwomba mtu msaada. Kama inawezekana, kuwa na simu yako ya mkononi.<br>• Elezea kuwa, maombi ni kule kuzungumza na Mungu. Mungu hajibu kwenye maongezi hayo lakini anasikia. Ana nguvu za kujibu maombi yetu.<br>• Kwenye habari ya leo, kuna kikundi cha marafiki walioombea jambo fulani la muhimu. |
| **FUNDISHA** | • Petro akiwa gerezani. ***(Matendo 12: 1-4)*** Mfalme Herode aliwachukia wafuasi wa Yesu. Yakobo aliuwawa. Muda mfupi baadaye, Petro akakamatwa na kutiwa gerezani. *Kumbuka wakati uliopita Petro alikuwa ametiwa tena gerezani.* ***(Matendo 4:3*** *– A7/ habari ya tatu)*<br>• Marafiki wa Petro waliomba. ***(Matendo 12: 5)*** *Jadili kwa nini hili lilikuwa ni jambo zuri zaidi la kufanya.*<br>• Huru kutoka gerezani. ***(Matendo 12:6-10)*** Ulikuwa usiku kabla ya kesi yake *(elezea umuhimu wa ule uamuzi wa kesi ile)*. Petro alikuwa amefungwa na minyororo katikati ya askari wawili lakini yeye alikuwa amelala usingizi mzito. Elezea jinsi gani Petro aliokolewa na malaika. Elezea kwa msisimuko na kwa undani ili kuwafanya watoto kushangaa jinsi gani mambo hayo yalitokea. Petro aliwaza labda alikuwa anaota.<br>• Petro akiwa nyumbani kwa rafiki zake. Mara tu Petro alipofika nje ya gereza kule njiani, akatambua kuwa, Mungua alikuwa amemuokoa. *Je, Petro alijihisi vipi wakati huo?* Moja kwa moja akaenda kwenye nyumba ya rafiki zake. ***(Matendo 12:11-17)*** Elezea Roda alivyomjibu mlangoni na walivyofanya. Je, wangestaajabu?<br>• *Jadili kuhusu mambo ambayo tunaweza kuyaombea. Kila wakati, Mungu anasikia maombi yetu na atayajibu kwa njia bora zaidi aijuaye Yeye.*<br>• *Inatupasa kukumbuka kumshukuru na kumsifu Mungu anapojibu maombi yetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Peter's miraculous escape from prison. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Yakobo 5:16***. Mstari huu unatuambia kwamba, maombi yetu yanaweza kuleta utofauti. Mungu anatumia maombi yetu kufanya kazi Yake. |
| **KUMBUKA** | • Ni nani aliyekuwa amemtia Petro gerezani?<br>• Mfalme Herode alikuwa tayari amemuua nani?<br>• Petro alikuwa anafanya nini Mungu alipomtuma malaika?<br>• Kwa nini marafiki wa Petro walikuwa wamekusanyika?<br>• Je, malaika alimwambia Petro afanye nini?<br>• Je, Petro alitokaje pale kwenye mlango wa gereza?<br>• Je, malaika alimwongoza Petro mpaka wapi kabla hajamwacha?<br>• Je, aliendа kwa nyumba ya nani?<br>• Ni nani aliyeenda mlangoni na kumwona Petro?<br>• Kwa nini Roda hakufungua mlango mara ya kwanza?<br><br>**Igiza:** Sehemu ambayo Petro anatoka gerezani inaweza kuigizwa na watu wawili. Mtoto mmoja kama Petro na yule mwingine kama malaika. Mtu mzima anaweza kunena maneno na watoto waigize tu. |

## A9 Habari ya kwanza

**Yakobo amdanganya ndugu yake – Habari hii inahusu kuwa na ubinafsi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Kuwa mbinafsi ni kujipa kipaumbele hata kama unawaumiza wengine.<br>• Kama Yakobo, sisi pia tunaweza kuwa wabinafsi na jambo hili ni dhambi mbele za Mungu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 25:28 au Wafilipi 2:3***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 25:19-34*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Je, unawajua mapacha wowote? Je, wako tofauti au wanafanana sura na tabia? Je, Umewahi kupigana na kaka, dada au wadogo zako?<br>• Je, inamaanisha nini kuwa na ubinafsi? Je, unaweza kufikiri kuhusu wakati ambao mtu unayemjua alikuwa mbinafsi na jambo hili likakuumiza?<br>• Habari hii inawahusu ndugu wawili waliokuwa hawapatani. Mmoja wao alijifikiria yeye tu hata akamdanganya kaka yake. |
| **FUNDISHA** | • Isaka na Rebeka walikuwa wanatarajia mapacha. Kabla mapacha hao hawajazaliwa, Mungu akamwambia Rebeka kuwa, yule mkubwa atamtumikia yule mdogo. ***(Mwanzo 25:19-23)***<br>• Mapacha wale walipozaliwa, ilikuwa wazi kuwa watakuwa tofauti sana. Esau ambaye alikuwa mkubwa alikuwa na ngozi yenye malaika na Yakobo alikuwa mlaini. ***(Mwanzo 25:24-26)*** Pia walifurahia vitu tofauti – Esau akawa mwindaji mzuri na Yakobo alipenda kukaa hemani. Kila mzazi alikuwa na mwana aliyempenda zaidi. Isaka alimpenda Esau lakini Rebeka alimpenda Yakobo. ***(Mwanzo 25:27-28)*** *Waambie watoto wafikiri kuhusu kuwa na vitu wavipendavyo zaidi.*<br>• Siku moja, Yakobo alikuwa anapika chakula cha dengu. Esau alikuwa ametoka mawindoni. Wasaidie watoto kufikiria kuhusu mazingira hayo – Esau alikuwa amechoka na mwenye njaa kali, ile harufu ya chakula kitamu! Ilimbidi Esau kula wakati huo! Lakini Yakobo alikuwa mjanja. Kwa haraka, akasema atampa chakula kama Esau atampa haki yake ya mzaliwa wa kwanza. *Elezea haki ya mzaliwa wa kwanza. Yule mtoto wa kiume wa kwanza wa familia alipata haki hiyo. Hii ilimaanisha kuwa, angekuwa kiongozi wa familia ile baba yake atakapofikiri. Pia, angepata utajiri wa baba yake mara dufu.*<br>• Esau hakuchukua muda wa kufikiri, alikuwa na njaa sana! Akamruhusu mdogo wake kumdanganya naye akauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa kupata chakula ***(Mwanzo 25:29-34)*** *Jadili matendo ya wana hao wawili. Je, Yakobo alikuwa na haki ya kumdanganya Esau na kuchukua haki yake ya mzaliwa wa kwanza? Je, ilikuwa sawa Esau kuuza haki yake ya uzaliwa wa kwanza kwa kupata sahani ya chakula?*<br>• *Je, unafikiri Mungu alifurahishwa na Yakobo na Esau?*<br>• *Mara nyingine, tunawaza tu kuhusu tunachokitaka kama vile Esau na Yakobo. Tunapokuwa na ubinafsi, tunatenda dhambi mbele za Mungu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** bibleforchildren.org - Jacob. FBI – Esau sells his birthright to Jacob. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Mwanzo 25:28 au Wafilipi 2:3*** |
| **KUMBUKA** | • Wale wavulana wawili kwenye habari waliitwa akina nani?<br>• Mwana yupi alikuwa wa kwanza?<br>• Taja mambo mawili yaliyowafanya wale wavulana kuwa tofauti.<br>• Haki ya mzaliwa wa kwanza ilikuwa nini?<br>• Kwa nini Yakobo alitaka kupata ile haki ya mzaliwa wa kwanza?<br>• Je, Yakobo alimdanganya Esau kwa njia gani?<br>• Je, tunajifunza nini kutoka kwenye habari hii? |

## A9 Habari ya pili

## Yakobo amdanganya baba yake – Habari hii inahusu jinsi Yakobo alivyodanganya.

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Rebeka na Yakobo walitaka kumdanganya Isaka.<br>• Kusema uongo/kudanganya ni dhambi machoni pa Mungu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 27:20 au Zaburi 32:***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 27:1-29*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Je, inamaanisha nini kusema uongo?<br>• Kwenye habari hii, Yakobo anamdanganya baba yake. Uongo wake unawaumiza sana baba na kaka yake.<br>• Je, unaweza kufikiri kuhusu habari zingine ambapo mtu amesema uongo na kumuumiza mtu mwingine? |
| **FUNDISHA** | • Isaka alikuwa mzee na kipofu. Alitaka kumbariki mwanawe Esau aliyekuwa mkubwa. Alitaka kufanya hivi kabla hajafa. Akimwambia Esau amuandalie chakula kizuri. ***(Mwanzo 27:1-4)*** *Elezea kuwa, kwenye wakati huo wa Biblia, baba angempa mtoto wake wa kwanza baraka kabla ya kufa.*<br>• Rebeka aliposikia kuwa Isaka alikuwa anajiandaa kumbariki Esau, wakiwa na Yakobo wakaanda njama ya kumdanganya Isaka ili ambariki Yakobo badala ya Esau. Rebeka akaandaa chakula kizuri na akamfunika Yakobo kwenye mikono yake kwa ngozi ya mwana –kondoo ili awe na malaika kama Esau. ***(Mwanzo 27:5-17)*** *Wakumbushe watoto kuwa, kila mzazi alikuwa na mwana ampendaye zaidi. Rebeka alimpenda sana Yakobo naye Isaka alimpenda sana Esau. Kila mmoja wao alitaka, mwana ampendaye zaidi apate baraka. Toa mfano wa upendeleo kama huo nyumbani au shuleni na kuwapa watoto fursa yakutambua kuwa siyo haki!*<br>• Yakobo akamletea Isaka chakula kile kizuri. Akamdanganya Isaka na kujifanya kuwa, yeye ni Esau. Isaka akashangaa kuwa Esau aliweza kupata chakula hiki kitamu kwa muda mfupi sana. ***(Mwanzo 27:18-20)***. *Je, unafikiri kuwa Rebeka alimpendeza Mungu? Je, ni kwa nini?*<br>• Isaka bado alikuwa na wasiwasi. Alitaka kujua, kweli huyo alikuwa ni Esau? Akataka kuwa na uhakika. Akaomba kugusa mikono yake kama ilikuwa na malaika. ... Kweli, mikono yake ilikuwa kama ya Esau lakini sauti ilikuwa kama ya Yakobo. Isaka akachanganyikiwa. Kisha Yakobo akadanganya tena na kumwambia baba yake kuwa, yeye ni Esau. ***(Mwanzo 27:21-24)***<br>• Isaka akala chakula ambacho Yakobo alikuwa amemletea. Alipomaliza akambariki Yakobo akifikiri kuwa alikuwa anambariki Esau. ***(Mwanzo 27:25-29)*** *Je, unafikiri Esau alijihisi vipi alipojua kuwa alikuwa amedanganywa?*<br>• *Kwa nini Mungu alituamuru tusiseme uongo?*<br>• *Fuata mfano wa Bwana Yesu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** bibleforchildren.org - Jacob. FBI – Jacob deceives Isaac. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Mwanzo 27:20 au Zaburi 32:2*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Isaka alimpenda mwana yupi zaidi?<br>• Rebeka alimpenda nani zaidi?<br>• Isaka alikuwa anataka kumfanyia nini Esau kabla hajafa?<br>• Je, Rebeka alitaka Esau apate baraka hizo? Je, ni kwa nini?<br>• Kwa nini Yakobo na Rebeka walimdanganya Isaka?<br>• Kwa nini Isaka hakutambua kuwa yule aliyembariki alikuwa Yakobo?<br>• Je, unafikiri kuwa Yakobo na Rebeka walimpendeza Mungu kwenye habari hii? Kwa nini hawakumpendeza? |

# <u>A9 Habari ya tatu</u>
## Yakobo akutana na Mungu – Habari hii inahusu Mungu anavyowajali watu.

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Tunaweza kumwamini Mungu kwa sababu anatimiza ahadi zake.<br>• Mungu anatujali.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 28:16 au Zaburi 86: 11***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 28:1-22*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Kumbusha watoto jinsi gani Yakobo alivyomdanganya Esau kwenye habari ya wiki iliyopita. Esau alikasirika sana na akataka kumuua Yakobo. Yakobo akaamua kuondoka pale nyumbani kwa muda.<br>• Waulize watoto kufikiri wao ni Yakobo. Je, wangejihisi vipi kama ingewalazimu kutoka nyumbani kwa sababu kama hii?<br>• Elezea watoto kuwa, hata kama Yakobo alikuwa ametenda mabaya, Mungu bado alikuwa anampenda na kumjali. Habari yetu ya leo inatuambia jinsi gani Mungu alijidhihirisha kwa Yakobo. |
| **FUNDISHA** | • Isaka akambariki Yakobo na kumpa maelekezo kutoka nyumbani na kwenda kwa familia ya mjomba wake Labani aliyeishi Padan- aramu. Alienda ili kupata mke wake huko. ***(Mwanzo 28: 1-5)***<br>• Akiwa kwenye safari yake, Yakobo alipumzika wakati wa usiku. Alitumia jiwe kama mto. *Waza hii ingekuwaje!* Alipokuwa amelala, akapata ndoto kuhusu ngazi liliyokuwa imesimama juu ya nchi na ncha yake imefika mbinguni. Malaika wa Mungu walikuwa wanapanda na kushuka kwenye nganzi ile. ***(Mwanzo 28: 10-12)***<br>• Mungu alikuwa amesimama juu ya ile ngazi. Akamwambia Yakobo kuwa atambariki na kumpa uzao mkubwa. Mungu akaahidi kuwa na Yakobo. Siku Moja, Mungu angemrudisha Yakobo nyumbani. ***(Mwanzo 28: 13-15)*** *Jadili ahadi ni nini. Je, kila mara tunatimiza ahadi zetu? Kwa nini hatutimizi? Elezea watoto kuwa, kila mara, Mungu anatimiza ahadi zake. Yeye ni mwenye nguvu zote na hasemi uongo.*<br>• Yakobo alipoamka, alijua kuwa mungu alikuwa mahali pale. *Elezea jinsi gani Yakobo aliogopa alipojua kuwa Mungu alikuwa pamoja naye mahali pale. Yakobo alikuwa amefanya mambo mengi ambayo hayakumpendeza Mungu lakini Mungu aliendelea kumjali!* Kisha akachukua lile jiwe alilokuwa amelitumia kama mto na kulimwagia mafuta. Akapaita mahali pale Betheli. Yakobo akaahidi kuwa, kama Mungu atakuwa naye na kumrudisha nyumbani, Mungu atakuwa Mungu wake. ***(Mwanzo 28:16-22)*** Yakobo bado alihitaji kujifunza kuwa Mungu anatimiza ahadi zake!<br>• *Sisi ni kama Yakobo kwa sababu tumefanya mabaya. Mungu anatupenda na kujali kila mmoja wetu kama alivyompenda Yakobo. Elezea kuwa alimtuma Mwana Wake afe msalabani kwa ajili yetu. Bwana Yesu ni kama "ngazi" inayotupeleka kwa Mungu na mbinguni ambapo ni nyumbani.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** bibleforchildren.org - Jacob. FBI – God speaks to Jacob in a dream. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Mwanzo 28:16 au Zaburi 86:11*** |
| **KUMBUKA** | • Kwa nini Yakobo alilazimika kutoka nyumbani?<br>• Kwa nini Yakobo alitumia jiwe kama mto?<br>• Yakobo aliona nini kwenye ndoto yake?<br>• Je, Mungu alimwambia nini Yakobo kwenye ndoto?<br>• Je, Mungu bado alimjali Yakobo hata kama alikuwa amefanya mambo mabaya hapo awali?<br>• Je, tutajuaje kuwa Mungu anatupenda?<br>• Je, Yakabo alifanya nini na lile jiwe?<br>• Je, Bwana Yesu ni kama "ngazi" kwa namna gani? |

**A9 Habari ya nne**

**Yakobo apata mke – Habari hii inahusu jinsi Yakobo alivyodanganywa na mjomba wake.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yakobo aliyekuwa mdanganyifu naye alidanganywa pia.<br>• Ni lazima tuwatendee wengine tunachotaka kutendewa.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 29:28 au Wagalatia 6:7***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 29:1-30*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Je, Umewahi kwenda kukaa na familia ambayo haujawahi kukutana nao hapo awali? Je, kukaa nao itakuaje? Au, toa mfano wako mwenyewe. Wakumbushe watoto kuwa, Yakobo alikuwa anaenda kukaa na mjomba wake Labani kule Padan- aramu.<br>• Watambulishe wahusika wapya kwenye habari hii; Labani na binti zake Lea na Raheli.<br>• Kwenye habari hii, Yakobo aligundua jinsi gani mtu anajihisi pale anapodanganywa. |
| **FUNDISHA** | • Yakobo alikuwa njiani kuelekea Padan-aramu. Mwisho wa safari yake akakutana na wachunga – kondoo kisimani. Wachunga-kondoo hawa walikuwa wanamjua mjomba wake – Labani. ***(Mwanzo 29:1-8)***<br>• Raheli aliyekuwa binti ya Labani akaja kisimani na kondoo wa baba yake. Yakobo akamsaidia kuwapa kondoo maji kwa kuondoa jiwe lililokuwa limefunika kisima. ***(Mwanzo 29:9-10)***<br>• Yakobo akamwambia Raheli yeye ni nani. Raheli akikimbia kumwambia baba yake na Laban akamwalika Yakobo akae nao nyumbani kwake. ***(Mwanzo 29:11-14)*** *Jaribu kufikiri kuhusu mazungumzo waliyokuwa nayo!*<br>• Yakobo akaanza kumfanyia Labani kazi. Ilimlazimu Yakobo kumfanyia labani kazi kwa miaka saba ili kumpata Raheli kama mke wake. Alikuwa tayari kufanya hivyo kwa sababu alimpenda Raheli. ***(Mwanzo 29: 15-20)***<br>• Lakini Labani akamdanganya Yakobo. Badala ya kumpa Raheli akampa Lea kuwa mke wake. ***(Mwanzo 29:21-27)*** *Je, Yakobo alijihisi vipi alipogundua kuwa amedanganywa? Waambie watoto wakumbuke jinsi gani Yakobo alikuwa amewadanganya wengine.*<br>• Yakobo alimwoa Raheli lakini ilimlazimu kufanya kazi kwa miaka mingine saba. ***(Mwanzo 29:29-30)*** Inaonekana kuwa Labani alikuwa amefaidika sana kupitia kwa Yakobo!<br>• *Je, unafikiri kuwa Yakobo alitubu wakati ambao aliwadanganya wengine?*<br>• *Wengine wanaweza kusema kuwa Yakobo alikuwa amepata kilichomfaa. Jadili ili kujua mawazo ya watoto kuhusu jambo hili.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** bibleforchildren.org - Jacob. FBI – Jacob is deceived at his wedding. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Mwanzo 29: 28 au Wagalatia 6: 7*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Labani alikuwa anaishi wapi?<br>• Binti wawili wa Labani waliitwa akina nani?<br>• Yakobo alimsaidiaje Raheli alipofika Padan-aramu?<br>• Yakobo alimpenda binti yupi?<br>• Je, Yakobo alisema angetumika kwa miaka mingapi ili kumwoa Raheli?<br>• Je, Labani alimdanganya Yakobo kwa njia gani?<br>• Je, Yakobo alimtumikia Labani kwa miaka mingapi zaidi baada ya kumwoa Raheli?<br>• Je, Yesu alisema nini kuhusu inavyotupasa kuwatendea wengine? |

## A10 Habari ya kwanza

**Stefano afa kwa ajili ya Bwana Yesu – Habari hii inahusu upendo mkubwa wa Stefano kwa ajili ya Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Stefano alimpenda Mungu na adui zake pia.<br>• Yesu alikuwa na Stefano alipokuwa akipigwa mawe na alikuwa anamsubiria mbinguni.<br><br>**Mstari muhimu:** ***1 Yohana 4:19***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 6:8-15, 7:54-60*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize watoto kuhusu wakati ambao walikuwa wamewasaidia wengine.<br>• Je, ungehisi vipi kama ulikuwa unajaribu kumsaidia mtu aliyekuwa hataki kusaidiwa? Je, kama wangekutukana au kukuumiza ungejihisi vipi?<br>• Habari ya leo kutoka kwenye Biblia inahusu mtu aliyewasaidia wengine. Tuangalie watu wale walimfanyia nini. |
| **FUNDISHA** | • Stefano alimpenda Bwana Yesu. Alifanya miujiza iliyowasaidia watu lakini Wayahudi wengine hawakumpenda na pia hawakumpenda Yesu. Kwa siri, waliamua kumdhuru na kumkomesha asiwaambie watu kuwa Yesu alikuwa amekufa kwa ajili yao. ***(Matendo 6:8-11)***<br>• Watu hawa wakasema uongo kuhusu Stefano na kumtenga na watu. Wakampeleka mahakamani ili waamue watamfanya nini. Pia wakawaweka mashahidi wa uongo kuhusu yale aliyokuwa anayasema. ***(Matendo 6:12-15)*** *Je, ungejihisi nini kama ungekuwa Stefano?*<br>• Hata kama walisema uongo kumhusu Stefano na Yesu, Stefano hakukasirika. Watu waliweza kuona kuwa Yesu alikuwa naye – Hata uso wake ukaonekana kama wa malaika. ***(Matendo 6:15)*** Stefano akamtetea Yesu lakini jambo hili liliwafanya watu wale kukasirika zaidi. ***(Matendo 7:54)*** Badala ya kuogopa, Stefano akatazama mbinguni na akamuona Yesu akimsubiria. ***(Matendo 7:55-56)*** *Je, Stefano alijihisi nini alipomwona Yesu?*<br>• Wale watu wakakasirika zaidi kwa sababu ya Stefano na wakakataa kumsikiliza. Wakampeleka Stefano nje ya mji wakampiga kwa mawe makubwa na kumuua. Walipokuwa wakifanya hivi, Stefano aliomba kuwa Yesu apokee roho yake na kuwasamehe watu wale kwa mambo waliyokuwa wanamfanyia. Kisha akakata roho. ***(Matendo 7:57-60)***<br>• *Kabla Stefano hajafa, alimwomba Yesu afanye jambo kwa adui zake – Kwa nini unafikiri alifanya hivi?*<br>• *Je, tutasamehewaje kwa mabaya tunayoyafanya?*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Stephen is martyred. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***1 Yohana 4: 19***. *Elezea kuwa, upendo wa Stefano kwa Bwana Yesu ulidhihirika alipokuwa tayari kufa kwa ajili Yake. Bwana Yesu alikuwa ameonesha upendo wake kwa Stefano kwa kufa msalabani kwa ajili yake.* |
| **KUMBUKA** | • Stefano alikuwa msaidizi kanisani. Je alikuwa anasaidia kwa njia gani?<br>• Je, kila mtu alimpenda Stefano? Kwa nini?<br>• Wale Wayahudi waliwageuza watu wawe kinyume na Stefano kwa njia gani?<br>• Je, Stefano alifanya nini waliposema uongo kumhusu yeye na Yesu?<br>• Je, Stefano aliona nini alipoangalia mbinguni?<br>• Wale watu walimfanyia nini Stefano?<br>• Je, Stefano aliomba nini?<br>• Je, tunaweza kusamehewa kwa kufanya nini? |

<u>A10 Habari ya pili</u>

**Filipo ahubiri Habari Njema – Habari hii inahusu Mwafrika kuamini Habari za Bwana Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Tunahitaji kumwamini Bwana Yesu ili tusamehewe dhambi.<br>• Mungu anatusaidia kuelewa sehemu zisizo rahisi za Neno Lake, Biblia.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 8:35***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 8:26-40*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize watoto jangwa ni sehemu ya namna gani. Je, linafananaje? Je, watu huishi jangwani? Je, kama ungeombwa kwenda jangwani kuongea na mtu usiyemjua, ungetii?<br>• Au, unaweza kukumbuka wakati ambao ulipata ugumu kuelewa kitu fulani, kwa mfano: Kitabu, swali kwenye somo la Hisabati? Je, ni nani aliyekusaidia? |
| **FUNDISHA** | • Filipo alimwamini Yesu na akahubiri Habari Njema ya Yesu kwenye miji. Siku moja, malaika akamwambia aende njia ielekeayo jangwani. *(Je, Filipo aliwaza nini kuhusu jambo hili?)* Elezea jinsi Filipo alivyoona gari la farasi likimjia. Ikawa gari lile lilikuwa limembeba mtu mmoja muhimu sana kutoka nchi ya Kushi (Ethiopia) aliyekuwa njiani akielekea nyumbani. *(Elezea Kushi ni wapi)* ***(Matendo 8:26-28)*** *Je,unafikiri huyu Mkushi alihitaji kusikia nini?*<br>• Kisha Roho Mtakatifu akamwambia Filipo amsogelee yule mtu. Alikuwa anasoma kwa sauti kitabu cha nabii Isaya kutoka kwenye Agano la Kale. Filipo akamwuliza kama alikuwa anaelewa kitabu hicho lakini yule mtu alikuwa hakielewi! ***(Matendo 8:29-31)***. Mstari mmoja ulikuwa unahusu Mtu mmoja ambaye angeuawa kama mwana –kondoo. *(Elezea kuwa mwana –kondoo ni mpole kweli anapopelekwa machinjioni.)* Filipo akamwelezea kuwa, mstari ule ulikuwa unamhusu Bwana Yesu akifa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. *(Elezea jinsi gani Yesu alikuwa tayari kufa)*<br>• Yule Mkushi akatambua kwamba alikuwa mwenye dhambi na alihitaji msamaha kutoka kwa Mungu. Bila kupoteza muda, akaamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili yake. ***(Matendo 8:32-35)***<br>• Filipo akambatiza kama ishara kuwa alikuwa amefanyika mfuasi wa Yesu *(Elezea ubatizo). Elezea mabadiliko na furaha iliyokuwa imeingia maishani mwake.*<br>• Roho Mtakatifu akampeleka Filipo sehemu nyingine kuhubiri Habari za Yesu. ***(Matendo 8:36-40)***<br>• *Mungu anataka kila mtu ajue kwamba Bwana Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Ongea kuhusu watu wanaotusaidia kuelewa Habari za Biblia. Inatupasa kushukuru kwa sababu tumesikia Habari Njema ya Yesu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Phillip and the Ethiopian Official. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Matendo 8:35*** |
| **KUMBUKA** | • Je, malaika alimwambia Filipo aende wapi?<br>• Yule mtu alikuwa anatoka nchi gani?<br>• Kwa nini Filipo alimsogelea?<br>• Lile somo la Biblia lilikuwa linahusu nini?<br>• Je, Yule mtu alifanya nini Filipo alipomwelezea kuhusu Yesu?<br>• Je, alibatizwa wapi?<br>• Je, alijihisi nini alipokuwa anasafiri kwenda nyumbani?<br>• Je, tunaweza kusamehewa dhambi zetu kwa namna gani? |

## A10 Habari ya tatu

**Sauli na nuru kali! – Habari hii inahusu Nguvu ya Mungu inayobadilisha maisha.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu anampenda kila mmoja na alikufa kwa ajili yetu sote, hata wale wanaomchukia.<br>• Ni Bwana Yesu tu mwenye nguvu za kubabilisha maisha yetu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***2 Wakorintho 5:17***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 9: 1-9*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Sauli alikuwa Myahudi aliyemchukia Yesu. Aliwachukia sana watu waliomfuata Yesu na akataka kuona wakiuawa. Elezea kuwa, Sauli alikuwepo wakati Stefano alipopigwa kwa mawe. (Kutoka kwenye habari ya kwanza)<br>• Waulize watoto kama wangependa Sauli awe rafiki yao? Je, ni kwa nini? |
| **FUNDISHA** | • Siku moja, Sauli akaondoka akielekea Dameski. Alikuwa anaenda kuwatafuta Wakristo ili kuwatia gerezani. ***(Matendo 9:1-2)*** *Jadili hisia na mawazo ya Sauli alipokuwa njiani akielekea Dameski.*<br>• Alipokuwa akielekea Dameski, kwa ghafla, akaona nuru kali imeangaza kote kote na akaanguka chini. *Tumia maneno aliyoambiwa Sauli na majibu yake. Elezea jinsi gani Sauli alikuwa anahisi sasa.* ***(Matendo 9:3-4)***<br>• Ile sauti ikajibu kuwa ni Yesu. *Elezea, Sauli alitambua nini sasa– Kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, Yu hai. Mawazo yake kumhusu Yesu hayakuwa sahihi muda wote huo!* Yesu akamwambia aende mpaka mji wa Dameski na ataambiwa cha kufanya. Wale watu waliokuwa na Sauli walishangaa sana kwani walisikia ile sauti lakini hawakumuona aliyekuwa akinena. ***(Matendo 9:5-7)***<br>• Sauli alipoinuka, alikuwa kipofu na ikabidi aongozwe hadi kwenye mji. Kwa siku tatu alikuwa kipofu na hakula wala kunywa chochote. ***(Matendo 9:8-9)*** *Je, unafikiria alihisi vipi kuwa kipofu?*<br>• *Elezea kwa nini Bwana Yesu alikutana na Sauli kwa njia hii. Wakumbushe watoto kuwa Sauli alikuwa anamchukia Yesu na wafuasi wake. Alitaka kuona kuwa wote wamekufa lakini Yesu alimpenda na alitaka awe mfuasi wake hata kama hakustahili. Bwana Yesu alitaka kubadilisha maisha yake kikamilifu.*<br>• *Tunahitaji Bwana Yesu atusamehe dhambi zetu na kutupa uwezo wa kuishi maisha mapya.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – The conversion of Saul. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***2 Wakorintho 5:17***, ilinganishe na maisha ya Sauli ya hapo awali na ukweli wa kuwa tukiwa “ ndani ya Yesu” maisha yetu yanabadilishwa na kufanywa upya. |
| **KUMBUKA** | • Sauli alikuwa anaenda wapi?<br>• Kwa nini alikuwa anaenda kwenye hii safari?<br>• Je, aliona nini?<br>• Je, alisikia nini?<br>• Je, ile sauti ilisema nini?<br>• Je, Sauli aligundua nini alipojua ni Yesu aliyekuwa anaongea naye?<br>• Je, sauli hakuweza kufanya nini kwa siku tatu?<br>• Ni nani pekee anayeweza kutupa uwezo wa kuishi maisha mapya? |

## A10 Habari ya nne

**Sauli akawa mtu aliyebadilishwa – Habari hii inahusu jinsi Mungu alivyomtumia Sauli kuwaambia wengine Habari za Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu anataka kutusaidia na anatuma watu kwetu tunapowahitaji.<br>• Kama Sauli, Mungu anabadilisha maisha ya watu hata leo na anaweza kuwafanya wawe watu muhimu kwake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 9:20***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 9:10-23*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Rudia ile sehemu ya kwanza ya habari ya Sauli – Je, unakumbuka "yule Sauli wa hapo awali" alivyokuwa? Je, wale wafuasi wa Yesu waliokuwa wanaishi Dameski walihisi nini kuhusu 'Sauli wa hapo awali"? (Waliogopa...)<br>• Mungu alitaka kuwaanda ili wamkubali yule Sauli "mpya" kama mmoja wa Famili Yake. Tuangalie kilichotokea.... |
| **FUNDISHA** | • Mungu akanena na Anania katika maono na akamwambia aende akamtafute Sauli. ***(Matendo 9:10-12)*** *Je, unafikiri Anania angependa kwenda? Kwa nini asingependa kwenda?*<br>• Anania aliogopa kwani alifikiri kuwa Sauli angemkamata au kumuua. Mungu alimwambia asiogope kwani alikuwa amemchagua Sauli kwa kazi maalum – kuwahubiria watu ambao hawajawahii kusikia Habari za Mungu. ***(Matendo 9: 13-16)***<br>• Anania alimtii Mungu na kwenda kwa Sauli. Akamwita ndugu *(elezea kwa nini walikuwa sasa ni ndugu)* na akamwambia kwamba alikuwa ametumwa na Bwana Yesu. Akamwekea mikono na Sauli akapata kuona tena. Sauli akajazwa Roho Mtakatifu . Akabatizwa na akala. ***(Matendo 9:17-19a)*** *Je, Sauli angejihisi vipi kuhusu kumtembelewa na Anania?*<br>• Baadaye, Sauli akakutana na wale wafuasi wengine wa Yesu kule Dameski. Mara hiyo, akaanza kuhubiri kuhusu Bwana Yesu. *Elezea mtazamo wa wale waliokutana na Sauli huko Dameski. Hawakutarajia Sauli angekuwa hivi!*<br>• Wale Wayahudi waliosikia kuhusu mabadiliko ya maisha ya Sauli hawakupenda habari aliyoihubiri kwa hiyo wakapanga kumwua. Ikamlazimu Sauli kutoroka Dameski kwa kushushwa ukutani akiwa kwenye kapu wakati wa usiku. ***(Matendo 9: 19-25)*** *Onyesha utofauti kwenye maisha ya Sauli na hali yake baada ya kuwa mfuasi wa Yesu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – The conversion of Saul. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Matendo 9:20*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Mungu alinena vipi na Anania?<br>• Kwa nini Anania aliogopa kwenda kwa Sauli?<br>• Kazi mpya ya Sauli ilikuwa ipi?<br>• Nini kilifanyika kwenye macho ya Sauli baada ya Anania kumwekea mikono?<br>• Sauli alipokea zawadi gani nyingine baada ya Anania kumtembelea?<br>• Je, Sauli alianza kufanya nini mara tu haya yalipotendeka?<br>• Kwa nini Sauli alitoroka akiwa kwenye kapu?<br>• Maisha yetu yatabadilikaje kabisa kama yale ya Sauli? |

## A11 Habari ya kwanza

**Paulo (Sauli) akiwa Antiokia – Habari hii inahusu kusaidia kwenye kazi ya Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Watu wanaomwamini Yesu wanaitwa "Wakristo".<br>• Mungu ana mpango maalum kwa ajili yetu tunapomwamini- Anataka tuwe wasaidizi wake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 11: 26***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 11: 19-26*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize watoto ni kwa njia gani wanaweza kusaidia – Je, wanaweza kumsaidia mwalimu kwa njia gani? Je, wangefanya nini kusaidia nyumbani kama mama angekuwa mgojwa?<br>• Elezea kuwa, habari ya leo inawahusu watu wawili waliosaidiana kwenye kazi ya Mungu. |
| **FUNDISHA** | • Habari Njema kuhusu Yesu ilikuwa inaenea na Kanisa la Mungu lilikuwa linakua. Baadhi ya waumini walienda kuishi kwenye mji uitwao Antiokia. Kule, waliweza kunena Habari Njema kwa watu ambao hawakuwa wameisikia habari hii na wengi wakamwamini Bwana Yesu. ***(Matendo 11:19-21)***<br>• Baadaye, Kanisa kule Yerusalemu likasikia kuhusu mambo makubwa yaliyokuwa yanatendeka Antiokia. *Je, wale waumini walihisi vipi? (walifurahi)* Wakaamua kumtuma mtu mmoja aitwaye Barnaba ili kuona zaidi jambo hilo. Akaenda Antiokia na akafurahi kuwapata watu wengi wapya walioamini. Barnaba alifanya yote awezayo kuwafundisha wale waumini wapya na kuwatia moyo kumpenda Bwana Yesu. ***(Matendo 11:22-24)*** *Je, Barnaba alikuwa mtu wa aina gani?*<br>• Barnaba alikuwa na shughuli nyingi huko Antiokia hata akahitaji msaidizi. Mungu akamkumbusha kuhusu Sauli, aliyekuwa amekutana naye miaka kadhaa iliyopita. Baada ya Sauli kukutana na Bwana Yesu, akarudi Tarso alikokuwa amezaliwa. Barnaba akaenda Tarso na kumleta Sauli huko Antiokia ili amsaidia kwenye kazi ya kuhubiri. ***(Matendo 11:25-26)***.<br>• *Elezea kuwa Antiokia palikuwa ni sehemu muhimu kwa Sauli /Paulo kwa sababu alianza kazi yake ya Umishonari huko. Ilikuwa ni kazi maalum ambayo Mungu alikuwa amempangia.* Sauli na Barnaba wakakaa Antiokia kwa mwaka mmoja wakiwafundisha watu walioamini. Wakati huo, watu waliomwamini Yesu Kristo kwa mara ya Kwanza waliitwa "Wakristo". ***(Matendo 11:26)***<br>• *Tunapomwamini Yesu, sisi pia tunakuwa "Wakristo".Tunashiriki Jina Lake! Mungu ana mpango maalum kwa Wakristo wote, kama alivyokuwa na mpango kwa ajili ya Paulo. Anataka Wakristo wawe wasaidizi Wake.*<br>• *Je, tunahitaji nini ili kuwa Wakristo?*<br>• *Kama sisi ni Wakristo, Je, Mungu anaweza kututumia kwa njia gani kama wasaidizi Wake?*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Paul in Cyprus. |
| **JIFUNZE** | Kama itafaa, fundisha na elezea Mstari muhimu – ***Matendo 11: 26*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Kanisa liliendelea kukua kwenye mji upi?<br>• Je, wale watu wa Yerusalemu walimtuma nani Antiokia?<br>• Je, Barnaba alifanya nini Antiokia?<br>• Je, baada ya muda mfupi Barnaba alihitaji nini?<br>• Je, Barnaba aliенda kumtafuta nani?<br>• Je, Sauli na Barnaba walikaa Antiokia kwa muda gani?<br>• Wale waliomwamini Yesu walipewa jina lipi?<br>• Je, Sauli alifanya kazi ya nani? |

**<u>A11 Habari ya pili</u>**

**Paulo (Sauli) akiwa Kipro – Habari hii inahusu kuwaambia wengine Habari za Bwana Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Tunahitaji kufanya uamuzi sahihi kwa kumwamini Yesu.<br>• Inatupasa kuwaambia wengine kuhusu Yesu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mathayo 28:19***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 13:1-12*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Wapange watoto wafanye kazi katika vikundi vya watu wawili na wafikirie kadri wawezavyo kuhusu Yesu.<br>• Elezea watoto kuwa habari ya leo inahusu Paulo (taja kuwa jina lake lilikuwa limebadilika), Barnaba na Yohana Marko, wakiwaambia watu Habari za Yesu. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja, Wakristo wa Antiokia walikusanyika pamoja. Paulo na Barnaba walikuwepo pia. Roho Mtakatifu akawadhihirishia wale viongozi wengine kuwa Barnaba na Paulo walikuwa wamfanyie Mungu kazi maalum. Baada ya kuliombea jambo hili, Barnaba, Sauli na Yohana Marko aliyekuwa binamu yake Barnaba wakapanda kwenye chombo na kuelekea kwenye kisiwa cha Kipro. ***(Matendo 13:1-4)***<br>• Walipofika kule, walitembea wakihubiri Habari Njema. Mahali paitwapo Pafo walikutana na mchawi mmoja aliyekuwa anamfanyia kazi liwali wa Kipro. Liwali yule alisikia kuhusu Paulo na Barnaba na akataka kukutana nao. Akasikiliza Neno la Mungu lakini Elima, yule mchawi akataka kumzuia asiamini. ***(Matendo 13:5-8)***<br>• Sauli alijua kuwa yule mchawi alikuwa anafanya kazi ya uovu. Sauli akiwa amejaa Roho Mtakatifu akamkazia macho na kumwambia kuwa alikuwa anafanya uovu na Bwana angemfanya kipofu. Baada tu ya Paulo kunena, Elima akawa kipofu na ilimlazimu kuzunguka –zunguka na kujaribu kupata mtu atakayemwongoza. ***(Matendo 13:9-11)*** *Elezea kuwa ni vibaya kumpinga Bwana Yesu.*<br>• Yule Liwali akaona ukuu wa nguvu za Mungu na akamwamini Yesu. ***(Matendo 13:12)***<br>• *Paulo, Barnaba, Yohana Marko na yule Liwali walifanya uamuzi mzuri kwa kumwamini Yesu. Elima alifanya uamuzi mbaya. Yesu anata pia sisi tumuamini.*<br>• *Kwa nini Ujumbe wa Yesu ndio ujumbe tu unaostahili?*<br>• *Je, unamjua mtu mwingine anayewaambia watu kuhusu Yesu kwenye eneo lingine?*<br>• *Je, unawezaje kuwaambia watu wengine kuhusu Yesu?*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Paul and Barnabas visit Cyprus. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Mathayo 28:19***. Elezea kuwa haya ni maneno ya Yesu kabla hajarudi mbinguni. Ulikuwa ni mpango Wake kuwa, watu wote kila mahali (wa mataifa yote) wasikie Habari Njema na kumwamini. |
| **KUMBUKA** | • Ni nani aliyewatuma Paulo na Barnaba wafanye ile kazi maalum?<br>• Ni nani aliyeambatana nao?<br>• Je, walisafiri vipi?<br>• Walikuwa wanaenda kwenye kisiwa gani?<br>• Je, walikutana na nani huko Pafo?<br>• Ni mtu gani kule Pafo aliyemwamini Mungu?<br>• Ni nini kilitendeka kwa yule mchawi?<br>• Ni nani aliyezungumza maneno ya Mstari muhimu wa somo la leo? |

## A11 Habari ya tatu

## Paulo akutana na Lidia – Habari hii inahusu mwanamke aliyemwamini Bwana Yesu.

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Kila amwaminiye Bwana Yesu ataokolewa.<br>• Tunaweza kuzungumza na Mungu tukiwa mahali popote na kuhusu kila kitu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 2:21***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 16:6-15*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize watoto waelezee kuhusu wakati ambao walienda kwenye safari ya mbali. Je, walienda wapi? Iliwachukua muda gani kwenda kwenye hiyo safari? Je, walimwona nani huko?<br>• Elezea kuwa habari ya leo inahusu Paulo na rafiki zake wakiwa safarini. |
| **FUNDISHA** | • Paulo na rafiki zake wawili, Sila na Timotheo, walisafiri kwa maili nyingi wakienda kwenye nchi moja hadi nyingine. Roho Mtakatifu akawaonesha ni wapi haswa Mungu alitaka waende. Haijalishi walikoenda, kila sehemu ilikuwa na watu wengi waliohitaji kusikia kuhusu Bwana Yesu. ***(Matendo 16:6-8)***<br>• Mwishowe wakafika kwenye mji uliokuwa ufukweni. Usiku huo, Paulo akapata maono ambapo mtu kutoka Makedonia aliwaomba akina Paulo waje huko na kuwasaidia watu wa sehemu hiyo. Paulo alijua kuwa Mungu alikuwa anawaonesha kwa uhakika sehemu waliostahili kwenda. ***(Matendo 16: 9-10)*** *Elezea kuwa Mungu alitaka watu wasikie kuhusu Yesu kwa hiyo akawatuma Paulo na rafiki zake kwenye mji huo. Haijalishi tunapoishi, Mungu anataka kila mtu asikie Habari Zake.*<br>• Kwa haraka wakapata mashua iliyokuwa inaelekea huko. Baadaye wakafika kwenye mji mkubwa uitwao Filipi. Siku ya Sabato, Paulo na rafiki zake wakaenda nje ya mji kando ya mto. Wakakutana na wanawake waliokuwa wamekuja kusali. ***(Matendo 16:11-13)*** Wale wanawake walikuwa wanamwomba Mungu. *Je tunaweza kuzungumza na Mungu tukiwa mahali gani? ( Elezea watoto kuwa tunaweza kuomba tukiwa sehemu yoyote)*<br>• Mmoja wa wale wanawake aliitwa Lidia. Alikuwa anauza nguo za rangi ya zambarau na alikuwa amemwamini Mungu kwa muda mrefu lakini alikuwa hajawahi kusikia kuhusu Mwana wa Mungu, Bwana Yesu. Lidia akasikiliza kwa makini kila kitu alichokisema Paulo. Alijua moyoni mwake kuwa, yote aliyoyasikia yalikuwa ni ya kweli na akamwamini Bwana Yesu. Alifurahi sana kwa kuwa Paulo alikuwa amekuja kwenye mji wake. ***(Matendo 16:14-15)*** Familia ya Lidia pia wakawa Wakristo. Wote walibatizwa na Lidia akawalika Paulo na rafiki zake wakae nyumbani kwake.<br>• *Je, tunaweza kuzungumza na Mungu kuhusu nini? (Waruhusu watoto wabuni baadhi ya mawazo na uwaelezee kuwa wanaweza kuongea na Mungu kuhusu chochote)*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Paul and Silas travel to Philippi. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Matendo 2:21***. *Elezea kuwa, kuliita Jina la Bwana kunamaanisha kumwomba atuokoe kutoka kwenye dhambi zetu. Hili ndilo jambo ambalo Lidia alifanya kwenye habari hii.* |
| **KUMBUKA** | • Taja mmoja wa marafiki wa Paulo.<br>• Ni nani aliyewaonesha sehemu ambayo Mungu alitaka waende?<br>• Nini kilitokea kwenye maono ya Paulo?<br>• Je, Paulo na rafiki zake walisafiri vipi walipokuwa wakielekea Makedonia?<br>• Je, Paulo na rafiki zake walikutana wapi na wale wanawake?<br>• Je, walikuwa wanafanya nini?<br>• Kazi ya Lidia ilikuwa ipi?<br>• Je, Lidia alifanya nini aliposikia kuhusu Yesu? |

## <u>A11 Habari ya nne</u>

**Paulo na Sila gerezani – Habari hii inahusu watu wengine waliookolewa.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Lazima tumwamini Bwana Yesu ili tuokolewe.<br>• Wakristo wana furaha kwa sababu wana Yesu kama Mwokozi wao.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 16: 31***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Matendo 16: 16-34*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize watoto ni nini ambacho huwafurahisha.<br>• Waambie watoto kuwa, kuna baadhi ya watu wenye furaha kwenye habari ya leo. Waambie wasikize kwa makini ili wajue ni akina nani ambao walikuwa na furaha.... |
| **FUNDISHA** | • Siku moja, Paulo na Sila wakiwa Filipi, walimsaidia msichana kijakazi. Waliwakasirisha sana waajiri wake na wale bwana wakawakokota Paulo na Sila mpaka sokoni na kunena uongo kuwahusu. ***(Matendo 16:16-21)*** *Jadili hisia za Paulo na Sila.*<br>• Paulo na Sila walipigwa na kutiwa gerezani. Yule mlinzi wa gereza akawafunga miguu kwa mkatale. ***(Matendo 16:22-24)*** *Je, unafikiri Paulo na Sila walihisi vipi?*<br>• Usiku wa manane wale wafungwa wengine waliwasikia Paulo na Sila wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu! Hata kama migongo yao ilikuwa na maumivu kutokana na kipigo walichopata, bado waliweza kumsifu Mungu. ***(Matendo 16:25)*** *Wafungua wengine wangefikiri nini?*<br>• Kwa ghafla kukatokea sauti nyingine. Kila kitu kikatetemeka. Milango ikafunguka na vifungo vya wote vikalegezwa. Hili lilikuwa ni tetemeko la ardhi. ***(Matendo 16:26)***<br>• Yule mlinzi akaamka na kuona kwamba milango yote ya gereza ilikuwa imefunguka. *Je, unadhani ni wazo gani lilimjia kwanza?* Paulo akamwambia asiwe na wasiwasi kwani wafungwa wote walikuwa pale ndani. ***(Matendo 16:27-28)***<br>• Yule mlinzi akamuuliza Paulo afanye nini ili aokolewe kwani alikuwa mwenye dhambi. Paulo akamjibu, "Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka." Paulo na Sila wakamwelezea yule mlinzi na familia yake kuwa Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zao. Yule mlinzi akawapeleka Paulo na Sila nyumbani kwake akawaosha vidonda vyao na kuwapa chakula. Ulikuwa ni usiku wa furaha sana kwa yule mlinzi na familia yake kwa sababu wote walimwamini Yesu. ***(Matendo 16:29-34)***<br>• *Akina nani walifurahi kwenye habari hii? Kwa nini walifurahi? (Watie moyo watoto wazungumze kuhusu Paulo na Sila pamoja na yule mlinzi na familia yake. Elezea watoto kuwa, watu hawa walifurahi kwa sababu Yesu alikuwa amewaokoa)*<br>• *Elezea watoto kuwa, tunahitaji kuokolewa kutoka kwenye dhambi zao. Inatupasa kumwamini Yesu kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu na alikufa kwa ajili yetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI- Paul and Silas in Prison. |
| **JIFUNZE** | Kama infaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Matendo 16:31*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Paulo na Sila walimsaidia nani?<br>• Je, ni nini kilitokea kwa Paulo na Sila?<br>• Je, Paulo na Sila walifanya nini usiku wa manane?<br>• Je, nini kilitokea walipokuwa wanaimba?<br>• Kwa nini yule mlinzi aliogopa baada ya lile tetemeko la ardhi?<br>• Je, yule mlinzi aliwauliza nini Paulo na Sila?<br>• Je, Paulo na Sila walimwambia nini?<br>• Je, yule mlinzi alifanya nini usiku huo?<br>• Je, tunajifunza nini kwenye somo hili? |

## A12 Habari ya kwanza

**Zakaria na Elisabeti – Habari hii inahusu Mungu kujibu maombi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu anajibu maombi.<br>• Maombi yanajibiwa kwa wakati wa Mungu, na sio kwa wakati wetu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 1:13***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 1:5-25*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize watoto kuhusu familia zao. Jadili nao kuhusu watoto kwenye familia zao au jamaa zao. Watoto wanawafanya watu wafurahi.<br>• Waulize watoto kuhusu kitu ambacho wangekipenda zaidi. Waruhusu waeleze kwa nini wangependa kitu hicho kitokee? Wanandoa kwenye habari hii walijihisi kitu kama hicho, walitaka kupata mtoto! |
| **FUNDISHA** | • Zakaria na Elisabeti walitamani sana kuwa na mtoto. Walipoendelea kuwa wazee, wengi wa marafiki zao walikuwa na watoto lakini wao walikuwa wenyewe tu. *Je, unafikiri walijihisi vipi? Ni nini ambacho Zakaria na Elisabeti walikuwa wamekosa kwa ajili ya kukosa watoto? Waruhusu watoto watoe maoni kulingana na hali yao au jamii zao.* ***(Luka 1:5-7)***<br>• Wakaamua kumwomba Mungu kuhusu jambo hilo. Walijua kuwa Mungu anajibu maombi! ***(Luka 1:13)*** *Taja kuwa, tunaweza kuomba kuhusu tatizo lolote tulilonalo.*<br>• Mungu alisikia Maombi yao na akatuma malaika akutane na Zakaria alipokuwa anahudumu hekaluni. *Je unafikiri Zakaria alihisi vipi malaika alipomtokea?* Malaika alimwambia asiogope na kisha akamwambia habari njema kuwa Elisabeti atapata mtoto ambaye jina lake ataitwa Yohana. ***(Luka 1:8-11)***<br>• Zakaria hakuamini habari hii aliyoambiwa. Alidhani kuwa, yeye pamoja na Elisabeti walikuwa wazee zaidi na wasingeweza kupata mtoto. Malaika akamwambia kwa sababu hakuamini ujumbe wa Mungu, atakuwa bubu hadi mtoto wao wa kiume atakapozaliwa. ***(Luka 1:18-20)***<br>• *Tunaweza kujifunza somo muhimu sana kutoka kwa Zakaria ... Tunapoomba, ni lazima tuamini kuwa Mungu atajibu maombi yetu.*<br>• *Fikiri baadhi ya mambo ambayo watu wanaweza kuombea leo!*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Zechariah is promised a son. (P) The birth of John the Baptist (I). |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Luka 1:13*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Zakaria alikuwa amemwoa nani?<br>• Je, walitaka nini?<br>• Je, Zakaria na Elisabeti walimwomba nani?<br>• Je, ni nani aliyekuja kukutana na Zakaria hekaluni?<br>• Je, Zakaria alijihisi nini malaika alipokutana naye?<br>• Je, ujumbe kutoka kwa malaika ulikuwa upi?<br>• Je, ni nini kilitokea kwa Zakaria kwa sababu hakuamini ujumbe ule?<br>• Tunapoomba, je ni jambo lipi muhimu ambalo linatupasa kufanya? |

## A12 Habari ya pili

**Mariamu na Gabrieli – Habari hii inahusu kuamini alichokisema Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mariamu alikubali ule ujumbe wa malaika hata kama kwake jambo hili lilionekana kama halingewezekana.<br>• Mungu anaweza kufanya mambo ambayo yanaonekana kana kwamba hayawezekani.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 1:37***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 1:26-38*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Rudia habari ya wiki iliyopita kuhusu ujumbe wa malaika ambapo Zakaria na Elisabeti wangepata mtoto. Muda mfupi baadaye, Mungu akamtuma malaika kufanya safari nyingine maalum. |
| **FUNDISHA** | • *Elezea utofauti wa Mariamu na Elisabeti.* Mariamu alikuwa mwanamwali aliyekuwa ameposwa kwa mtu aitwaye Yusufu aliyeishi kwenye mji wa Nazareti. Siku moja akatembelewa na malaika aitwaye Gabrieli. ***(Luka 1:26-27)*** *Wasaidie watoto kuelewa kuwa hili halikuwa jambo la kawaida na kwa hali ya ubinadamu, Mariamu aliogopa.*<br>• Malaika akamwambia asiogope. Akasikiliza kwa makini Gabrieli alipokuwa anamwambia kuwa atapata Mtoto wa kiume. Mariamu alichanganyikiwa kidogo; alikuwa bado hana mume. Yule malaika akamwambia kuwa, Mungu Roho Mtakatifu atampa huyu Mtoto maalum. Alitakiwa ampe Jina, Yesu. ***(Luka 1:29-34)***<br>• Yesu angekuwa mkubwa kuliko kila mtoto ambaye aliwahi kuzaliwa. Angekuwa, Mwana wa Mungu. Ilikuwa ngumu kuelewa lakini malaika alimwambia Mariamu kuwa hakuna kisichowezekana kwa Mungu. ***(Luka 1: 35-37)***<br>• Mariamu aliamini ujumbe ule alioambiwa. Mariamu alikuwa tayari kuwa sehemu ya mpango mkuu wa Mungu wakumtuma Mwana wake ulimwenguni. Kuzaliwa kwa Yesu kulikuwa muujiza wa ajabu. ***(Luka 1: 38)***<br>• *Je, Umewahi kuahidiwa jambo ambalo halikuwa rahisi kuamini?*<br>• *Je, kwa nini Mariamu alimwamini malaika? Mungu anataka kila mmoja wetu aweze kumwamini kama Mariamu alivyomwamini.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – An angel visits Mary. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Luka 1: 37***. *Wape watoto muda wafikirie kuhusu baadhi ya mambo ambayo "hayangewezekana" ambayo Mungu aliyafanya kwenye Biblia? Msifu kwa kuwa Mungu mkuu!* |
| **KUMBUKA** | • Je, Mariamu aliishi wapi?<br>• Je, Mariamu alikuwa ameposwa na nani?<br>• Jina la malaika aliyemtembelea Mariamu aliitwa nani?<br>• Kwa nini Mariamu alichanganyikiwa kidogo kuhusu ule ujumbe wa malaika?<br>• Je, yule mtoto angekuwa maalum kwa njia gani?<br>• Je, Mariamu alifanya nini kuhusu ule ujumbe?<br>• Je, ni kwa jinsi gani Mariamu ni mfano mzuri wa sisi kuiga?<br>• Mambo gani "yasingewezekana" pasipo Mungu? |

<u>**A12 Habari ya tatu**</u>

**Kuzaliwa kwa Yohana – Habari hii inahusu ahadi za Mungu kutimia.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alitimiza ahadi yake kwa Zakaria na Elisabeti.<br>• Mungu anatimiza ahadi zake kwetu pia.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 1:76***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 1:57-80*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Jadili jinsi gani mtu anaweza kujihisi kama hawezi kuongea kwa miezi kadhaa. Wakumbushe watoto kuwa, hili lilitokea kwa Zakaria alipokosa kuamini ujumbe wa malaika.<br>• Inapendezaje kama ni siku ya Krismasi asubuhi au siku ya kukumbuka kuzaliwa kwako, unapopata zawadi ambayo ulikuwa unatarajia? Hivi ndivyo Zakaria na Elisabeti walijihisi mwana wao mdogo wa kiume alipozaliwa kama vile alivyoahidi malaika. Ulikuwa ni wakati maalum. |
| **FUNDISHA** | • Mtoto alipozaliwa, jamaa zake na majirani walitaka aitwe Zakaria kama baba yake. Lakini Elisabeti akawaambia kuwa jina lake ni Yohana. ***(Luka 1:57-60)*** *Kwa nini Elisabeti aliwaambia mtoto ataitwa Yohana?*<br>• Zakaria alipoulizwa jina la mtoto wake wa kiume, aliandika kuwa, "Jina lake ataitwa Yohana." ***(Luka 1:62-63)***<br>• Mara tu, akaweza kuongea tena. Zakaria akashukuru na kumsifu Mungu. *Kwa nini Zakaria alifanya hivi? Mungu alikuwa ametimiza ahadi yak. Zakaria akajawa na furaha kwa sababu ya kuzaliwa kwa mwana wake na alijua kuwa, Mungu atatenda mambo makuu zaidi!* Kila mmoja alishangazwa na alichokiona. ***(Luka 1:64-66)***<br>• Yohana alikuwa mtoto maalum. *Je, ni kwa sababu gani? Wakumbushe watoto kuwa wazazi wake walikuwa wamemsubiria kwa miaka mingi na cha muhimu zaidi ni kuwa, alikuwa aandae njia kwa ajili ya ujio wa Bwana Yesu.*<br>• *Mungu pia atatimiza ahadi zake kwetu. Taja baadhi ya ahadi alizotupa kwenye Biblia.*<br><br>**Kamilisha somo la Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Birth of John the Baptist. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Luka 1:76***. Elezea kuwa, mstari huu ni sehemu ya ule wimbo wa Zakaria wa kumsifu Mungu. |
| **KUMBUKA** | • Je, ni nani alikuwa mume wa Elisabeti?<br>• Je, kwa nini hakuweza kuongea?<br>• Je, majirani walitaka mtoto aitwe nani?<br>• Je, kwa nini Zakari na Elisabeti walimwita Yohana?<br>• Je, Zakaria aliweza kuongea muda gani?<br>• Je, Yohana alikuwa afanye kazi gani maalum?<br><br>***Tengeneza:*** Watoto wanaweza kutengeneza vikadi vidogo vya kutangaza kuzaliwa kwa mtoto Yohana. |

<u>A12 Habari ya nne</u>

**Kuzaliwa kwa Yesu – Habari hii inahusu Mungu kumtoa Mwana wake.**

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kuwa:<br>• Yesu ni Mwana wa Mungu aliyekuja kuwa Mwokozi wetu.<br>• Inatupasa kumshukuru Mungu kwa upendo wake mkuu hata akamtuma Bwana Yesu duniani.<br><br>Mstari muhimu: Luka 2:7<br>Habari kwenye Biblia: Luka 2:1-7</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>• Elezea jinsi gani mipango inaweza kubadilika dakika za mwisho. Toa mfano ambao ni mwafaka kwenye watoto unaowafundisha. Mfano huo unaweza kutoka kwa watoto au kwako.<br>• Elezea kuwa, wakati ulikuwa unawadia wa Mtoto wa Mariamu kuzaliwa. Ingekuwa bora zaidi Mtoto huyu kuzaliwa Nazareti ambapo ndio sehemu walikotokea Yusufu na Mariamu, lakini .....</td></tr>
<tr><td>FUNDISHA</td><td>• Kaisari Augusto alitoa amri kuwa watu wote warudi walipozaliwa ili wajiandikishe. Iliwalazimu Yusufu na Mariamu kusafiri hadi Bethlehemu. (Luka 2:1-5) Waelezee watoto safari ilikuwa na umbali gani – Takriban maili 80 au safari ya siku nne. Je, ilikuwaje kwenda safari ya namna hii? (Kwa watoto wa daraja la pili, unaweza kuwaambia kuwa, ulikuwa ni mpango wa Mungu Mtoto huyu azaliwe Bethlehemu!)<br>• Walipofika Bethlehemu, mji ulikuwa umejaa na walikosa nafasi kwenye nyumba ya wageni. Wakati wa Mtoto huyo kuzaliwa ulipofika iliwalazimu kupumzika kwenye sehemu ya kulaza wanyama. (Luka 2:6-7)<br>• Mtoto Yesu alipozaliwa, alivikwa nguo za kitoto na akalazwa kwenye hori ya kulia ng’ombe. (Luka 2:6-7) Kwa nini Yesu alivisha nguo kama hizo na kulazwa kwenye hori ya kulia ng’ombe? Wasaidie watoto kuheshimu ukuu wa Mtoto aliyezaliwa mahali pa chini. Unaweza kulinganisha kuja kwa mtoto huyu na jinsi gani mtoto anakuja kwenye jamii mnayoishi.<br>• Hapajawahi kuwa na Mtoto mwingine kama Yesu. Yeye ni Mwana wa Mungu. Alikuwa tayari kuacha mbingu na kuzaliwa hapa ulimwenguni ili atukomboe kutoka kwenye dhambi zetu. (Mathayo 1:21)<br>• Inatupasa kukumbuka kuwa siku ya Krisimasi inahusu kuzaliwa kwa Yesu na inatupasa kumshukuru Mungu kwa upendo wake wa kumtuma Mwokozi.<br><br>Kamilisha somo la Biblia.<br>Onesha: tafuta kwenye mtandao wa FBI – The birth of Jesus, also PowerPoint www.bibleforchildren/the birth of Jesus.</td></tr>
<tr><td>JIFUNZE</td><td>Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – Luka 2: 7</td></tr>
<tr><td>KUMBUKA</td><td>• Je, ni nani aliyekuwa ameolewa na Yusufu?<br>• Je, Mariamu na Yusufu waliishi wapi?<br>• Je, Yusufu na Mariamu walisafiri hadi wapi?<br>• Kwa nini Yusufu na Mariamu walikuwa Bethlehemu?<br>• Kwa nini walipumzika kwenye sehemu ya kulaza wanyama?<br>• Mtoto Yesu alilazwa wapi?<br>• Je, ni nini kilimfanya Yesu awe mtoto maalum?<br>• Je, kwa nini tunamhitaji Mwokozi?</td></tr>
</table>

# Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**MASOMO YA DARAJA LA KWANZA:**
- Kurasa moja (au mbili kwenye kijitabu) kina sehemu za kupaka rangi au kujaza maneno machache kila wiki.
- Alama kumi zimewekwa kwa kila wiki na alama 40 kwa kila mwezi.
- Watoto wanaotumia masomo ya Daraja la kwanza hawatarajiwi kuwa wanajua kusoma vizuri. Hivyo basi, tunatarajia wazazi/ walezi/ viongozi wa madarasa kuwasaidia.
- Tumeweka alama 2 kwa kila jibu na hizo zilizobaki ili kuwa kumi ni kwa ajili ya maswali ya kupaka rangi. Jumla alama 10 kwa kila somo/ habari.

**MASOMO YA DARAJA LA PILI:**
- Kurasa mbili kila wiki.( au nne kwenye vijitabu)
- Habari ya Biblia ipo kwenye somo. Watoto/ wanafunzi wanapaswa kupata baadhi ya maneno kwenye somo, kupaka rangi, kukamilisha Mstari muhimu na kadhalika.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kila mwezi masomo yanapokamilishwa kwa usahihi.

**KUSAHIHISHA MASOMO YA WAKATI NA BIBLIA**

**VITU VYA KUTUSAIDIA TUNAPOSAHIHISHA**
Waalimu wanaombwa kwanza:
- Kuangalia kila somo na kusahihisha ipasavyo.
- Toa alama kama ulivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia wino wa rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini hakuna alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama nusu kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uandike kwenye nafasi uliyopewa kwa ajili hiyo.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.

Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**DARAJA LA KWANZA**
**Maoni ya jumla**
“Neema – Ninafurahi kuwa umeanza masomo haya na natumai unayafurahia. Nimependa sana ulivyopaka rangi.
“Je, huwa unaenda shule? Niambie kuhusu shule yako. Ninatarajia kusikia kutoka kwako siku za karibuni.”
“Hongera sana Pendo! Umepaka rangi kwa ustadi kweli! Je, ilikuwa vigumu kupaka rangi ndani ya picha tu? Ulikosea kidogo ulipokuwa unapaka rangi kwenye baadhi ya sehemu za somo la mwisho.”

**Maoni ya Kiroho**
“Umefanya vyema sana Faraja! Jairo alikuwa na furaha kubwa Yesu alipomsaidia.”
“Jibu zuri sana! Habari ya kifo cha Yesu inahuzunisha lakini cha kufurahisha ni kwamba, alifufuka tena.”

**DARAJA LA PILI**
**Maoni ya jumla**
“Jibu zuri sana Wema!– “Ninauhakika kuwa, walimu wako wanafurahia sana kazi zako huko shuleni!”
“Debora, naona kuwa tutasherehekea siku yako ya kuzaliwa hivi karibuni. Je, una maandalizi yoyote ya siku hiyo? Je, ni maadalizi gani? Uwe na siku njema!”
“Umejitahidi kweli. Lakini kuna makosa madogo. Usisahau kuhakiki majibu yako kila mara. Mtoto mzuri!”

**Maoni ya Kiroho**
“Napenda ulivyompaka rangi Mtoto Yesu akiwa horini. Je, si inapendeza sana Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni kwa ajili yetu?”
“Napenda sana rangi ulizozitumia! Ilimbidi Zakaria kulipa gharama ya kutoamini maneno ya Mungu. Hakukosa kuamini maneno ya Mungu tena.”
“Majibu mwafaka kweli! Mtu aliyekutana na Filipo kule jangwani alienda akiwa na furaha kweli. Alisikia na kuamini Habari Njema za Yesu.”

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK 1186004

Toleo la 01/2020